# Découvrez qui vous êtes vraiment

Par Brik V. Eyre
*des soixante-dix*

# Jua Wewe ni Nani Hasa

Na Mzee Brik V. Eyre
*Wa Sabini*

Conférence générale d’octobre 2025

*Où que nous en soyons sur le chemin du disciple, notre vie changera fondamentalement si nous comprenons mieux qui nous sommes vraiment.*

*Bila kujali wapi tulipo kwenye njia ya uanafunzi, maisha yetu kimsingi yatabadilika ikiwa tutaelewa sisi ni kina nani hasa.*

Il y a quelques années, notre fille a vécu une expérience profonde en mission. Avec son autorisation, j’aimerais vous lire un passage de ce qu’elle nous avait écrit cette semaine-là :

« Hier, une membre qui revient depuis peu à l’Église nous a demandé de venir chez elle le plus vite possible. Quand nous sommes arrivées, nous l’avons trouvée par terre. Elle pleurait de manière incontrôlable. Entre deux sanglots, elle nous a dit qu’elle avait perdu son travail, qu’elle allait être expulsée de son appartement et qu’elle allait donc se retrouver, une fois de plus, sans abri. »

Notre fille a ensuite écrit : « J’ai commencé à feuilleter frénétiquement mes Écritures pour y trouver quelque chose, quoi que ce soit, qui pourrait l’aider. Alors que je recherchais le parfait verset, je me suis demandé : ‘Qu’est-ce que je suis en train de faire ? Ce n’est pas ce que le Christ ferait. Je ne peux pas résoudre ce problème, mais je sais qu’elle est une véritable fille de Dieu et elle a besoin de mon aide.’ J’ai alors fermé mes Écritures, je me suis agenouillée à côté d’elle et l’ai prise dans mes bras pour pleurer avec elle, jusqu’à ce qu’elle soit prête à se relever et à affronter cette épreuve. »

Une fois cette femme réconfortée, notre fille a alors utilisé les Écritures pour lui faire comprendre la réalité de sa nature divine et lui enseigner l’une des vérités les plus fondamentales de notre existence : nous sommes des fils et des filles bien-aimés de Dieu, un Dieu qui a une compassion parfaite pour nous et qui est prêt à nous aider tandis que nous nous relevons.

Miaka kadhaa iliyopita, binti yetu alikuwa na uzoefu wa kupendeza kwenye misioni yake. Kwa idhini yake, ninashiriki sehemu ya kile alichotuandikia wiki ile:

“Jana, muumini aliyerudi Kanisani baada ya kutohudhuria kwa muda mrefu alituomba tumtembelee haraka iwezekanavyo. Tulipofika, tulimkuta kwenye sakafu, akilia sana. Akiwa analia machozi, tuligundua kuwa alikuwa amepoteza kazi yake, alikuwa akitakiwa kuondolewa kutoka kwenye nyumba yake aliyokuwa akiishi, na kwa mara nyingine tena, atakuwa asiye na makazi.”

Binti yetu aliendelea: “nilianza kwa haraka haraka kupekua maandiko, nikijaribu kupata kitu—chochote kile ili kumsaidia. Wakati nikitafuta mstari maalum, nilifikiria, ‘Ninafanya nini? Hiki sicho ambacho Kristo angefanya. Hili sio tatizo ambalo ninaweza kulitatua, lakini huyu ni binti halisi wa Mungu anayehitaji msaada wangu.’ Hivyo, nilifunga maandiko yangu, nikapiga magoti pembeni yake, na kumkumbatia wakati tukilia kwa pamoja, mpaka alipokuwa tayari kusimama na kukabiliana na jaribu hili.

Baada ya dada huyu kuwa amefarijiwa, binti yetu kisha alitumia maandiko kujaribu na kumsaidia kuelewa uhalisia wa thamani yake takatifu na kumfundisha moja kati ya kweli za msingi za kuwepo kwetu duniani—kwamba sisi ni wana na mabinti wapendwa wa Mungu, Mungu ambaye anahisi huruma kamilifu kwa ajili yetu wakati tunaposumbuka na yuko tayari kutusaidia wakati

Il est révélateur que le premier point de doctrine enseigné par nos missionnaires est que Dieu est notre Père céleste aimant. Toutes les autres vérités reposent sur la compréhension fondamentale de notre véritable identité.

Susan H. Porter, présidente générale de la Primaire, a enseigné : « Lorsque vous savez et comprenez avec quel amour parfait Dieu vous aime, vous, son enfant, cela change tout. Cela change la vision que vous avez de vous-même lorsque vous commettez des erreurs. Cela change ce que vous ressentez quand des choses difficiles se produisent. Cela change votre vision des commandements de Dieu. Cela change votre vision des autres et votre capacité de faire changer les choses. »

Ce changement est illustré par l'expérience de Moïse lorsqu'il a parlé face à face avec Dieu. Au cours de cette conversation, Dieu a enseigné à plusieurs reprises à Moïse son héritage divin, en disant : « Moïse, […] tu es mon fils. » Dieu a expliqué à Moïse qu'il avait été créé à l'image de son Fils unique. Moïse a compris clairement qui il était, qu'il avait une œuvre à accomplir et qu'il avait un Père céleste aimant.

Après cette expérience, l'adversaire est venu le tenter et s'est immédiatement adressé à lui en disant : « Moïse, fils de l'homme. » C'est une arme courante et dangereuse dans l'arsenal de l'adversaire. Notre Père céleste nous rappelle constamment et avec amour que nous sommes ses enfants, tandis que l'adversaire essaie toujours de nous étiqueter en fonction de nos faiblesses. Mais Moïse avait déjà appris qu'il était plus qu'un « fils de l'homme ». Il a demandé à Satan : « Qui es-tu ? Car voici, je suis un fils de Dieu. » De même, lorsque nous sommes confrontés aux difficultés de la condition mortelle ou lorsque nous avons l'impression qu'on essaie de nous étiqueter en fonction de nos faiblesses, nous devons rester forts dans la connaissance de notre véritable identité. Nous devons chercher l'approbation des cieux, et non des hommes. Ce faisant, nous pourrons, nous aussi, déclarer avec assurance : « Je suis enfant de Dieu. »

Dans une réunion spirituelle mondiale pour les jeunes adultes, notre cher président Nelson a déclaré : « Qui êtes-vous ? En tout premier

tunapo simama tena wima.

Ni ya kuleta umaizi kwamba kanuni ya kwanza ya fundisho ambalo wamisionari wetu wanafundisha ni kwamba Mungu ni Baba yetu Mpendwa wa Mbinguni. Kila ukweli wa kimatokeo hujenga kwenye msingi wa uelewa wa sisi ni kina nani hasa.

Susan H. Porter, Rais Mkuu wa Watoto, alifundisha: "Unapojua na kuelewa jinsi gani kwa ukamilifu unapendwa kama mtoto wa Mungu, hilo hubadilisha kila kitu. Linabadilisha namna unavyohisi kuhusu wewe binafsi wakati unapofanya makosa. Linabadilisha jinsi unavyohisi wakati mambo magumu yanapotokea. Linabadilisha mtazamo wako juu ya amri za Mungu. Linabadilisha mtazamo wako juu ya wengine, na juu ya uwezo wako wa kuleta tofauti."

Badiliko hili lina kielelezo wakati tunaposoma kuhusu uzoefu alioupata Musa wakati akizungumza na Mungu uso kwa uso. Wakati wa mazungumzo hayo, Mungu alirudia kumfundisha Musa kuhusu utakatifu wa urithi wake, akisema, "Musa, … wewe ni mwana wangu." Mungu alifafanua kwamba Musa alikuwa ni mfano wa Mwanawe wa Pekee. Musa alipata kuelewa dhahiri kuwa yeye alikuwa nani, kwamba alikuwa na kazi ya kufanya, na kwamba alikuwa na Baba mpendwa wa Mbinguni.

Baada ya tukio hili, mjaribu alikuja kumjaribu na mara moja alimuita kwa kusema "Musa, mwana wa mtu."Hii ni silaha ya mara zote na hatari iliyoko kwenye ghala la adui. Wakati Baba yetu wa Mbinguni mara zote na kwa upendo hutukumbusha kuwa sisi ni watoto Wake, adui daima atajaribu kutupa majina kwa kutumia madhaifu yetu. Lakini Musa tayari alikuwa amejua kwamba yeye alikuwa ni zaidi ya "mwana wa mtu." Alimtamkia Shetani, "Wewe ni nani? Kwani tazama, mimi ni mwana wa Mungu."Vivyo hivyo, wakati tunapokabiliwa na changamoto za maisha ya duniani au wakati tunapohisi kama mtu fulani anajaribu kutupatia jina kwa kutumia udhaifu wetu, tunahitaji kusimama imara katika uelewa wa ukweli wa sisi ni nani. Tunapaswa kutafuta uthibitisho kutoka juu, na si kutoka pembeni. Tunapofanya hivyo, nasi pia tunaweza kutamka kwa uthabiti, "mimi ni mtoto wa Mungu."

Katika ibada ya ulimwenguni kote kwa ajili ya vijana waseja, Rais Russell M. Nelson alifundisha: "Hivyo wewe ni nani? Kwanza na zaidi

lieu, vous êtes un enfant de Dieu, un enfant de l'alliance et un disciple de Jésus-Christ. Si vous vous attachez à ces vérités, notre Père céleste vous aidera à atteindre votre but ultime de vivre éternellement en sa sainte présence. »

Ce n'est pas une coïncidence si, dans l'Écriture probablement la plus répétée, Dieu nous rappelle notre relation avec lui. Parmi tous les noms par lesquels il pouvait être identifié dans la prière de Sainte-Cène, il a demandé à être appelé « Dieu, Père éternel».

Quand nous serons parvenus à la connaissance de notre véritable identité, nous croirons plus fermement que notre Père céleste aimant a préparé un plan pour que nous retournions vivre avec lui. Patrick Kearon a enseigné : « Le plan merveilleux de notre Père, ce plan 'fabuleux', a été conçu pour vous ramener à votre foyer céleste,paspour vous empêcher de revenir. […] Dieu vous poursuit sans relâche. » Réfléchissez-y un instant : notre Père tout-puissant et aimant « vous poursuit sans relâche ».

Où que nous en soyons sur le chemin du disciple, notre vie changera fondamentalement si nous comprenons mieux qui nous sommes vraiment. J'aimerais vous présenter deux manières d'approfondir cette compréhension.

## Premièrement, la prière

Au début de son ministère dans la condition mortelle, le Sauveur a été emmené dans le désert pour « être avec Dieu». Peut-être qu'au lieu de simplement faire nos prières, nous devrions prendre suffisamment de temps pour réellement communier avec Dieu et « être avec [lui] » chaque jour.

J'ai découvert que la qualité de mes prières s'améliore lorsque je prends quelques minutes pour me préparer à parler à mon Père. Les Écritures nous montrent que c'est un modèle qui fonctionne. Que ce soit Joseph Smith, Néphi, les fils d'Hélamanou Énos, tous ont médité et réfléchi avant leur communication avec Dieu. Énos a dit que son âme était affamée tandis que les paroles de son père pénétraient profondément son cœur. Chacun de ces exemples nous enseigne la nécessité de nous préparer spirituellement pour le temps que nous consacrerons chaque jour à « être avec Dieu ».

Le Sauveur a dit aux Néphites : « Mais quand tu pries, entre dans ta chambre, ferme ta porte, et prie ton Père. »

ya yote, wewe ni mwana wa Mungu, mwana wa agano na mfuasi wa Yesu Kristo. Unapokumbatia kweli hizi, Baba yetu wa Mbinguni atakusaidia kufikia lengo lako kuu la kuishi milele katika uwepo Wake mtakatifu."

Si kwa bahati kwamba katika maandiko yanayojirudia sana, Mungu hutukumbusha uhusiano wetu na Yeye. Katika majina yote ambayo Angeweza kutambulishwa nayo kwenye sala ya sakramenti, Yeye amechagua kuitwa "Mungu, Baba wa Milele."

Tunapokuja kujua ukweli sisi ni akina nani, tutaamini zaidi kwamba Baba yetu mpendwa wa Mbinguni ametoa mpango kwa ajili yetu wa kurudi kuishi Naye tena. Mzee Patrick Kearon alifundisha: "Mpango mzuri wa Baba Yetu, hata 'mpango Wake wa kupendeza', umesanifiwa ili kukurudisha wewe nyumbani,siokukuacha wewe nje. … Mungu anaweka juhudi endelevu kukutafuta."Fikiria kuhusu hilo kwa muda—Baba yetu mpendwa mwenye nguvu zote anaweka "juhudi endelevu kukutafuta wewe."

Bila kujali wapi tulipo kwenye njia ya uanafunzi, maisha yetu yatabadilika kwa kiasi kikubwa ikiwa tutaelewa sisi ni kina nani hasa. Ninaweza kupendekeza njia mbili ambazo kwazo tunaweza kulielewa hili kwa kina.

## Kwanza, Sala

Wakati Mwokozi alipoanza huduma Yake duniani, aliongozwa kwenda nyikani ili "kuwa na Mungu."Pengine tunapaswa kuondoa mawazo yetu kwenye kusema tu sala zetu na kuyapeleka kwenye kuchukua muda wa kutosha wa kuzungumza kwa dhati na "kuwa na Mungu" kila siku.

Nimegundua kwamba ubora wa sala huongezeka wakati ninapotumia dakika chache kujiandaa kuzungumza na Baba yangu. Maandiko yanatuonyesha kwamba mfumo wa aina hii hufanya kazi. Iwe Joseph Smith;Nefi, wana wa Helamani;au Enoshi, wote wana aina fulani ya mfumo wa kutafakari na kujichunguza kabla ya mawasiliano yao yaliyorekodiwa na Mungu. Enoshi alisema kwamba nafsi yake ilipata njaa wakati maneno ya baba yake yalipozama kwa kina moyoni mwake.Kila moja ya mifano hii hutufundisha hitaji la kujiandaa kiroho kila siku, "kuwa na Mungu."

Kwa Wanefi, Mwokozi alielekeza, "Lakini wewe unaposali, ingia kwenye chumba chako kidogo, na wakati umefunga mlango wako, sali

Que ce soit dans une chambre ou ailleurs, le principe est de trouver un endroit où vous pouvez être seul pour prier, calmer votre âme et ressentir les inspirations du « murmure doux et léger». Nous nous préparons en méditant sur les choses pour lesquelles nous sommes reconnaissants et sur les questions ou les préoccupations dont nous aimerions parler à notre Père. Nous devons nous efforcer de ne pas prier de manière mécanique, mais de vraimentparleravec notre Père, si possible à voix haute.

Je sais que, dans le chaos de notre vie, quand nous nous occupons d'enfants en bas âge ou quand nous courons d'une réunion à l'autre, nous n'avons peut-être pas le luxe de nous retirer dans un endroit calme pour bien nous préparer, mais les prières silencieuses, rapides et faites dans l'urgence, peuvent être beaucoup plus marquantes lorsque nous avons fait l'effort d'« être avec Dieu» plus tôt dans la journée.

Certaines personnes n'ont pas prié depuis longtemps et d'autres ressentent que leurs prières n'ont pas été entendues. Je vous promets que votre Père céleste vous connaît, vous aime et veut que vous lui parliez. Il veut communiquer avec vous. Il veut que vous vous souveniez de votre identité.

Jeffrey R. Holland a récemment enseigné : « Quel que soit le nombre de prières que vous faites déjà, priez davantage. Quelle que soit l'intensité de vos prières, priez avez plus de ferveur. »

En plus d'accroître la fréquence et la ferveur de nos prières, l'étude quotidienne du Livre de Mormon et le culte au temple contribueront à préparer notre esprit à recevoir la révélation. Si nous nous efforçons d'améliorer la qualité de notre communication avec notre Père céleste, il nous bénira afin que nous ressentions plus profondément que nous sommes ses enfants.

## Deuxièmement, parvenir à la connaissance que Jésus est le Christ

La plus grande manifestation de l'amour de notre Père céleste pour nous, ses enfants, est le fait qu'il a envoyé son Fils, notre Sauveur personnel, pour nous aider à retourner à lui. C'est la raison pour laquelle nous devons connaître le Christ.

Il y a plusieurs années, alors que j'étais président de pieu, j'ai envoyé une recommandation pour qu'un frère soit servant des ordonnances

kwa Baba yako"

Iwe ni kwenye chumba kidogo au chumba cha kulala, kanuni iliyopo ni kupata mahali ambapo unaweza kuwa peke yako ili kusali, kuruhusu nafsi yako kuwa tulivu, na kuhisi misukumo ya "sauti ndogo tulivu."Tunaweza kujiandaa kwa kutafakari kuhusu vitu ambavyo tuna shukrani navyo na kwa ajili ya dukuduku au maswali ambayo tungependa kupeleka kwa Baba. Tunapaswa kujitahidi kutokuwa na aina ya sala ya kujirudia rudia, lakinituzungumzena Baba yetu, kwa sauti kama inawezekana.

Ninatambua kwamba changamoto za maisha yetu, wakati tunaposumbuka na watoto wachanga au kuharakisha mikutanoni tunaweza tusiwe na chumba kidogo cha kifahari na maandalizi yafaayo—lakini sala hizo za kimya kimya, za haraka, na dharura zinaweza kuwa za muhimu zaidi wakati tunapokuwa tumeweka juhudi ya "kuwa na Mungu"mapema katika siku.

Kunaweza kuwa na baadhi ambao hawajasali kwa muda mrefu au wengine ambao hawajahisi kwamba sala zao zinasikiwa. Ninawaahidi kwamba Baba yenu wa Mbinguni anawajua, anawapenda, na anataka kusikia kutoka kwenu. Anataka kuwasiliana nanyi. Anataka mkumbuke ninyi ni akina nani hasa.

Rais Jeffrey R. Holland hivi karibuni alifundisha, "bila kujali ni kwa bidii kiasi gani unasali, sali zaidi. Bila kujali unasali kwa bidii kiasi gani, sali kwa bidii zaidi."

Kama nyongeza kweye ongezeko na utakatifu wa sala zetu, kujifunza Kitabu cha Mormoni kila siku na kuabudu hekaluni kutaandaa mawazo yetu kwa ajili ya ufunuo. Tunapojitahidi kuboresha mawasiliano yetu na Baba yetu wa Mbinguni, Yeye atatubariki tujisikie zaidi kwamba tu watoto Wake.

## Pili, Kutambua kuwa Yesu ni Kristo

Dhihirisho kuu la upendo wa Baba yetu wa Mbinguni kwetu kama watoto Wake ni uhalisia kwamba Yeye alimtuma Mwanawe, Mwokozi wetu binafsi, ili kutusaidia kurudi nyumbani. Hivyo, tunapaswa kumjua Yeye.

Miaka kadhaa iliyopita, wakati nikihudumu kama rais wa kigingi, niliwasilisha pendekezo kwa ajili ya kaka kuhudumu kama mhudumu wa

au temple. Après avoir expliqué qu'il serait un excellent servant des ordonnances, j'ai appuyé par inadvertance sur « Ne pas approuver » en voulant soumettre la recommandation. Après avoir essayé en vain d'annuler l'envoi du message, j'ai appelé le président du temple et lui ai dit : « J'ai fait une terrible erreur. » Sans hésiter, ce bon président de temple m'a dit : « Frère Eyre, il n'y a rien que vous ayez fait qui ne puisse être pardonné et finalement corrigé. » Quelle vérité puissante. En effet, Jésus est « puissant à sauver».

En 2019, des changements importants ont été apportés aux questions de la recommandation pour le temple. Précédemment, on vous demandait si vous aviez le témoignage que Jésus-Christ est le Sauveur et le Rédempteur. Désormais, on vous demande si vous avez le témoignage du rôle de Jésus-Christ en tant quevotreSauveur et Rédempteur. L'expiation de Jésus-Christ ne fonctionne pas seulement pour autrui. Elle fonctionne pour vous et pour moi. Il est mon Sauveur. Il est votre Sauveur. Individuellement. Ce n'est que par lui que nous pouvons, vous et moi, retourner auprès de notre Père.

Par conséquent, frères et sœurs, recherchons-le. Étudions sa relation divine avec le Père et avec chacun de nous. Faisons l'expérience du cantique de l'amour rédempteur qui nous parvient personnellement par l'intermédiaire de notre Rédempteur lorsque nous nous repentons. En apprenant à connaître « celui qui est puissant à sauver», nous comprendrons qu'en tant qu'enfants de Dieu, nous sommes sa joie, sa priorité absolue et que chacun de nous mérite vraiment d'être sauvé.

Je témoigne que nous avons un Père céleste aimant. Lorsque nous parviendrons à connaître cette vérité éternelle par la prière fervente, la révélation personnelle et en venant à Jésus-Christ, nous pourrons déclarer avec assurance, maintenant et à jamais : « Je suis enfant de Dieu. » Au nom de Jésus-Christ. Amen.

ibada za hekaluni. Baada ya kufafanua uzuri wa namna ambavyo mhudumu huyu wa ibada za hekaluni angekuwa, pasipo kukusudia nilibonyeza "Usimpitishe" na pendekezo langu liliwasilishwa. Baada ya kujaribu bila mafanikio kurudisha pendekezo lile, nilimpigia simu rais wa hekalu na kusema "nimefanya kosa kubwa." Pasipo kusita, Rais huyu mwema wa hekalu alisema "Rais Eyre, hakuna ambacho umefanya kisichoweza kusamehewa na hatimaye kusahihishwa." "Ni ukweli mkuu ulioje. Hakika, Yesu Kristo ana "uwezo wa kuokoa."

Mwaka 2019, kulikuwa na mabadiliko makubwa kwenye maswali ya kibali cha kuingia hekaluni. Kabla ya hapo, moja ya swali liliuliza ikiwa ulikuwa na ushuhuda kuhusu jukumu la Yesu Kristo kama Mwokozi na Mkombozi. Sasa linauliza ikiwa una ushuhuda kuhusu jukumu lake kama Mwokozi na Mkomboziwako. Upatanisho wa Yesu Kristo si tu unafanya kazi kwa wengine; unafanya kazi pia kwako na kwangu. Yeye ni Mwokozi wangu. Yeye ni Mwokozi wako. Kila mmoja binafsi. Ni kupitia Yeye pekee wewe na mimi tunaweza kurudi kuishi na Baba yetu.

Hivyo, akina kaka na akina dada, acheni tumtafute Yeye. Acheni tujifunze uhusiano Wake mtakatikfu na Baba na kwa kila mmoja wetu. Acheni tupate uzoefu wa wimbo wa upendo wa ukombozi ambao huja binafsi kwa kila mmoja wetu kupitia Mkombozi wetu wakati tunapotubu. Wakati tunapokuja kumjua "yeye anayeweza kuokoa,"tutakuja kuelewa kwamba sisi, kama watoto wa Mungu ni shangwe Yake, fokasi Yake kuu zaidi, na hakika kila mmoja ni mwenye kustahili kuokolewa.

Ninashuhudia kwamba tunaye Baba mpendwa wa Mbinguni. Tupatapo kujua ukweli huu wa milele kupitia sala ya dhati, ufunuo binafsi, na kumuendea Yesu Kristo, tunaweza sasa na daima kwa ujasiri kutamka "mimi ni mtoto wa Mungu." Katika jina la Yesu Kristo, amina.